BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSIANA NA TAARIFA YA AFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu (S.W) ambaye ametujaalia afya njema na uzima tukaweza kukutana siku hii ya leo katika Baraza hili kutekeleza majukumu yetu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwaombea shifaa wale wote wanaosumbuliwa na maradhi mbali mbali wapone kwa haraka ili nao waweze kutekeleza majukumu yao kwa lengo la kuijenga nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Pia napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa Hotuba hii, kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na mashirikiano niliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wa Kamati sambamba na maoni na ushauri wao walionipatia katika kipindi chote cha utekelezaji wa kazi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais - Fedha na Mipango, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara pamoja na taasisi zote za Serikali zilizofika mbele ya Kamati na kutoa majibu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuendelea naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Asha Abdallah Mussa | Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Fatma Ramadhan Mandoba | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii katika kufanikisha kazi zake inasaidiwa kwa karibu na Sekretarieti ya Kamati inayoundwa na Makatibu wanne kama ifuatayo:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Abass Vuai Moh'd | Katibu |
| 2. Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 3. Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti imefarajika sana na utekelezaji wa baadhi ya maagizo iliyoyatoa ambayo pamoja na mambo mengine, yalilenga kukuza ufanisi wa bajeti zetu katika ukusanyaji mapato, nidhamu katika matumizi sambamba na usimamizi mzima wa miradi ya maendeleo. Aidha, yapo baadhi ya maeneo ambayo Kamati haijaridhika na utekelezaji wake na inasisitiza yaendelee kufanyiwa kazi zaidi ili kuhakikisha mipango ya Serikali inaleta tija iliyokusudiwa. Mathalan, katika baadhi ya maeneo Kamati iliarifiwa kuwa utekelezaji wa maagizo hayo haujaanza au umeanza siku za karibuni wakati Kamati ilitoa maagizo yake tokea mwezi Februari mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika**, Miongoni mwa maagizo hayo ambayo utekelezaji wake si wa kuridhisha ni pamoja na agizo la Bodi ya Mkopo ya Elimu ya Juu Zanzibar la kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha watumishi wa umma waliokosa udhamini wa masomo katika taasisi zao na agizo la Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar kuingiziwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo sasa naomba niende moja kwa moja kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na taarifa ya utekelezaji wa maagizo iliyowasilishwa mbele ya Kamati na taasisi mbali mbali za Serikali. Katika taarifa hiyo, kulikuwa na maagizo mengi kwa taasisi hizo lakini katika hotuba hii tutayagusia maagizo machache ambayo Kamati imeona iyawekee msisitizo.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa maagizo hayo ni agizo la Kamati la kuitaka Serikali kuhakikisha kwamba, takwimu zinazokusanywa na Tume ya Mipango zinakuwa na uhalisia na kuakisi hali halisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu agizo hilo, Kamati iliarifiwa kuwa bado kuna mapungufu ya wataalamu wa takwimu katika sekta mbali mbali. Kutokana na mapungufu haya, Kamati inaishauri Serikali kupanga mpango wa muda mrefu wa kuongeza wataalamu wa takwimu nchini pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kuchakatia taarifa zinazokusanywa sambamba na kutumia teknolojia ya kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ndiyo yenye jukumu la kuwapatia mikopo wanafunzi wanaohitaji kujiendeleza katika fani mbali mbali za elimu ya juu. Katika utekelezaji wa agizo la Kamati kuhusiana na kuwakopesha watumishi wa umma ambao wanakosa fursa ya kupata ufadhili wa kimasomo katika taasisi zao wanazozifanyia kazi, Kamati haijaridhishwa na majibu yaliyoletwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Afisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora bado zipo katika hatua ya kuandaa mapendekezo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza mapendekezo hayo kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuwawezesha watumishi wa umma wanaokosa ufadhili katika taasisi zao kupata fursa ya kujiendeleza kimasomo ndani ya muda mfupi ujayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar haina jengo lake la kudumu na kwa sasa wamekodiwa ofisi katika eneo la Kwa Mchina, Kamati inasisitiza juu ya kupatiwa jengo lao la kudumu ili kuepusha usumbufu wa kuhama kila baada ya muda.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa maagizo ya Kamati kuhusiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Kamati inaipongeza Wizara katika utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH) kwa kufikia hatua kubwa ya utekelezaji wake. Aidha, Kamati inaisisitiza Wizara kujitahidi kukamilisha Mpango Mkuu wa Uvuvi Zanzibar ili uweze kusaidia katika kuendeleza zaidi mchango wa sekta ya uvuvi katika Pato la Taifa pamoja na kuhakikisha shughuli za uvuvi zinaendelea kuratibiwa vyema nchini na kuzuia shughuli zote za uvuvi zinazoweza kupelekea uharibifu wa rasilimali za bahari.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Wizara pia ina jukumu la kufahamu takwimu zinazohusiana na uvuvi, pamoja na jitihada wanazozichukua katika ukusanyaji wa takwimu hizo, Kamati inaitaka Wizara kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa takwimu hizo ili ziweze kuhifadhiwa na kunufaisha jamii kwa mahitaji yao mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipokea utekelezaji wa agizo la Shirika la Bandari Zanzibar la kufanyiwa kazi changamoto ya upungufu wa vifaa vya kufanyia kazi ambayo ni ya muda mrefu na inachangia kwa kiasi kikubwa kutokupatikana kwa ufanisi bandarini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa agizo hilo, Kamati imeelezwa kuwa Shirika limeshaagiza vifaa vya aina 10 ambapo miongoni mwa vifaa hivyo vimeshafika na vyengine vilivyobaki vinatarajiwa kufika ifikapo mwezi wa Disemba, 2022. Kamati

inasisitiza vifaa hivyo vipatikane ndani ya muda uliyopangwa ili visaidie katika kuimarisha huduma na kuvutia wafanyabiashara wengi kuleta mizigo yao nchini jambo litakalochangia kuongezeka kwa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPRA), Kamati iliagiza Mamlaka kusimamia mpango wa mafunzo kwa watendaji. Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa mpango huo kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wake kunakosababishwa na kutopatikana kwa fedha. Hivyo, Kamati inaitaka Afisi ya Rais – Fedha na Mipango kuipatia Mamlaka fedha kwa mujibu wa sheria na taratibu ili iweze kuendeleza mpango huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine Kamati iliishauri Serikali kuandaa eneo maalum kwa ajili ya kutunzia taarifa za mafuta na gesi. Utekelezaji wa agizo hili umepangwa kufanyika katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo Serikali imepanga kiasi cha Shilingi za Tanzania Bilioni 5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kituo maalum la kuhifadhia taarifa (Data Center). Pamoja na mipango hiyo, Kamati inataka kufahamu ujenzi wa kituo hicho utaanza katika robo gani ya mwaka wa huu wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Mamlaka kufanya utafiti na kujifunza ujenzi wa vituo mbali mbali vya kuhifadhia taarifa ili hatimae Mamlaka ipate wazo la ujenzi wa kituo kinachozingatia mazingira na mahitaji yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Kamati yangu imeridhika nalo ni juhudi zilizochukuliwa na Serikali kupitia Kitengo cha Madeni kinachosimamiwa na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango kuwa na ushiriakiano wa karibu na Kitengo cha Madeni cha Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kufanya usuluhishi wa Deni la Taifa na kupata taarifa inayoonesha uwiano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilikiagiza Kitengo cha Madeni kuzipatia mafunzo taasisi za Serikali ili kupata uelewa mpana wa taratibu za kukopa na kuomba dhamana katika madeni. Kamati imeelezwa kuwa tayari mafunzo yameshatolewa kwa badhi ya Taasisi

za Serikali. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, mafunzo haya yaendelee kwa taasisi nyengine zilizobaki. Aidha, Kamati inaunga mkono juhudi zilizochukuliwa na Serikali za kuandaa mfumo wa kuweka kumbukumbu za madeni ambao utasaidia katika kuainisha kwa wakati taarifa zote za madeni kwa pande zote mbili za muungano.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka zinazosimamia mapato yaani Bodi ya Mapato Zanzibar pamoja Mamlaka ya Mapato Tanzania – Zanzibar, Kamati iliagiza kuandaliwa mifumo ya kielektroniki ambayo itasaidia katika ukusanyaji wa mapato na kuweza kuzuia mianya ya uvujaji wa makusanyo hayo. Katika kutekeleza agizo hilo, Kamati imearifiwa kuwa tayari mifumo hiyo imekamilika na taratibu za kuwapatia elimu wananchi juu ya namna ya utumiaji wa mifumo hiyo inaendelea. Kamati inasisitiza mifumo hiyo isimamiwe kwa umakini ili kuleta tija iliyokusudiwa kwa kuongeza mapato na pia kuzuia kudukuliwa kwa mifumo hiyo ili wabadhirifu wa mali za umma wasipate mwanya wa kuvujisha mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza maagizo ya Kamati kuhusiana na Wizara ya Afya, Kamati inaipongeza Wizara katika utekelezaji wa kusimamia upatikanaji wa fungu maalum la fedha kwa ajili ya kituo cha uchukuaji wa sampuli za UVIKO 19 ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kupitia agizo hilo, Wizara ilipata ufadhili kutoka Global Fund na kuweza kununua vifaa pamoja na kufanya mafunzo kwa wafanyakazi wa Maabara ya Binguni kwa upande wa Unguja na Wawi kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA), Kamati ilishauri kuandaa mikakati madhubuti itakayoelekeza masharti na muda wa kurejesha mikopo ambayo inakopwa na wajasiriamali. Hii imetokana na kutokurudishwa kwa wakati kwa mikopo hiyo. Katika kutekeleza hili, SMIDA ilisitisha huduma hiyo ya mikopo na hatimae kuelekezwa huduma hii kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya SMIDA kusitisha huduma za mikopo, Kamati inaomba kupatiwa tathmini halisi ya taarifa za mikopo hiyo pamoja na wadaiwa. Aidha, Kamati inaitaka SMIDA kuchukua hatua za kufuatilia mikopo hiyo na watakaokuwa hawakulipa

hatua za kisheria zichukuliwe.

**Mheshimiwa Spika**, Eneo jengine ambalo Kamati ilitoa maagizo ni katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kuhusiana na mifumo wanayoitumia kukusanyia mapato ya vyombo vya moto vinavyoingia katika maegesho ya viwanja vya ndege ni kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kuvuja kwa mapato hayo. Kamati imeelezwa kuwa kwa sasa mfumo unaotumika umeimarika kwa kuwa umeandaliwa utaratibu wa kuwasilisha kadi eneo la kulipia ambayo itasoma muda uliotumia katika eneo hilo kabla ya kutoka. Baada ya malipo mtumiaji atakabidhiwa risiti ya kielekrtoniki na kuruhusika kutoka eneo hilo. Kamati inaipongeza hatua hii, na kuitaka Mamlaka kudhibiti mfumo huo ili kuepusha kuvuja kwa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Programu mbali mbali, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo kulingana na hatua iliyofikiwa katika miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa utekelezaji wa Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Boosting Inclusive Growth for Zanzibar - Big Z), Kamati ilibaini kuwepo kwa mapungufu makubwa katika utekelezaji wa mradi huu kama vile kuwepo kwa matumizi makubwa ambayo hayaakisi uhalisia wa majengo na miundombinu iliyojengwa. Hivyo, Kamati iliiagiza Serikali iweke mikakati maaalum ya kuhakisha thamani ya fedha inapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa agizo hilo, Kamati imeelezwa kwamba Afisi ya Rais – Fedha na Mipango inafanya usimamizi wa karibu kupitia kamati zinazosimamia mradi huo ili lengo la Mradi liweze kufikiwa. Kamati yangu inaendelea kusisitiza kwamba kuwepo na usimamizi bora wa rasilimali fedha katika utekelezaji wa miradi ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa utalii una mchango mkubwa katika uchumi wa nchi, utekelezaji wa miradi inayohusiana na utalii inahitaji rasilimali za kutosha na usimamizi mzuri. Katika Mradi wa Uimarishaji wa Utalii kwa Wote, Kamati ilibaini kuwa nguvu

inayotumika katika kuwekeza miradi kupitia sekta hiyo ni ndogo na kuishauri Serikali kuipa kipaumbele katika kuingiza fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa agizo linalohusiana na kubuni miradi mikubwa inayoleta tija katika sekta ya utalii, Kamati inakubaliana na hatua iliyofikiwa na Serikali ya kubuni miradi mikubwa ikiwemo Mradi wa Uimarishaji wa Mji Mkongwe, Mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria na Mradi wa Diversification of Tourism Product kwa Unguja na Pemba na inaisisitiza Wizara kusimamia vyema miradi iliyobuniwa na kuendelea na jitihada za kuibua miradi mengine mikubwa ambayo itaimarisha sekta ya utalii. Aidha, Kamati inaomba kupatiwa tathmini ya utekelezaji wa miradi hiyo iliyobuniwa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar, Kamati iliishauri Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuangalia vyanzo vya maji vilivyopo katika maeneo ya Mradi iwapo vinakidhi kupokea mabomba yanayotarajiwa kuwekwa. Kamati imearifiwa kuwa, Mamlaka katika kutekeleza ushauri huo, wamekagua mabomba ya maji yanayotumika kwenye mradi na kubaini kuwa zinaendana na uzalishaji wa maji katika vyanzo hivyo pamoja na presha ya maji. Kamati inaendelea kuweka msisitizo kwa Mamlaka kuhakikisha inatekeleza shughuli za uwekaji wa miundombinu ya maji kwa haraka ili kazi za usambazaji wa maji kwa wananchi nazo zifanyike kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mradi wa Uchimbaji wa Visima Zanzibar – Ras El Khaimah, Kamati ilishauri juu ushirikishwaji wa wadau katika kila hatua ya utekelezaji, kuwepo kwa timu ya ufundi (technical team) katika utekelezaji wa mradi, kuwekwa makubaliano ya mapema baina ya taasisi husika na jamii juu ya uchangiaji wa gharama za miradi itakayosimamiwa na wananchi itakapomalizika pamoja na kuendelezwa kwa visima vilivyokuwa havijakamilika na kuvihuisha ili viwanufaishe wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili, Kamati imebaini kwamba bado hakujawa na ushirikishwaji wa kutosha wa wadau kama Mamlaka inayoeleza.

**Mheshimiwa Spika,** Kwenye Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Elimu na Mradi wa Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali, Kamati iliagiza ujenzi wa vituo vitano vya mafunzo ya amali bila kuchanganya na miradi mengine kwa kuzingatia bajeti, uhitaji wa vituo kwa maeneo yenye uhitaji pamoja na usimamizi madhubuti wa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua zinazochukuliwa na Wizara kwenye utekelezaji wa agizo hilo, kwa kutekeleza miradi yote kwa mujibu wa mikataba ilivyosainiwa, jambo litakalosaidia katika usimamizi mzuri wa fedha za miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Kamati yangu imeona itowe msisitizo ni katika Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji Zanzibar, Kamati iliiagiza Wizara ya Kilimo, Maliasili na Umwagiliaji Maji kuwa makini na miradi ambayo gharama zake zitahitaji marekebisho mbali mbali pamoja na kumuwajibisha mshauri elekezi kwa kushindwa kushauri vyema kwenye ujenzi wa misingi ya kupitishia maji katika bonde la Mlemele.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ilizozichukua za kumuwajibisha mshauri elekezi, lakini pia inaendelea kuisisitiza Wizara kuongeza umakini kwenye miradi ambayo gharama zake zinafanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Shirika la Umeme (ZECO) kuhusiana na utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme Zanzibar (CBMP) na Mradi wa Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZEST), Kamati ilishauri kuwepo na muendelezo katika utekelezaji wa miradi hii. Jambo hili ni kutokana na changamoto ya kutoendelezwa vizuri kwa baadhi ya miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefarijika na hatua zilizochukuliwa na Shirika katika kuhakikisha kuwa miradi inakuwa endelevu kwa kutoa mafunzo ya usimamizi wa miundombinu pamoja na kufanya matengenezo ya miundombinu hiyo ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutekeleza kwa wakati agizo la Kamati linahusiana na kubadilisha usimamizi na uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama kutoka Afisi ya Rais kwenda kwa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA). Hatua hii itasaidia kupunguza gharama kubwa ya uendeshaji wa mradi huu kutokana na ZICTIA kuwa na wataalamu wenye weledi wa usimamizi na uendeshaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliiagiza Serikali kupitia Idara Maalum za SMZ kufanya ufuatiliaji wa madeni yote yanayodaiwa na Viwanda vya Ushoni wa Nguo na Viatu – KVZ na kuhakikisha yanalipwa ili kunusuru kuzorota kwa shughuli za uendeshaji wa viwanda hivyo. Hata hivyo, licha ya Idara Maalum za SMZ kuorodhesha madeni yote na kuyapeleka kwa wahusika lakini bado hakujaanza hatua zozote za ulipaji wa madeni hayo. Kamati inaisisitiza tena Serikali kulitafutia ufumbuzi suala hili kwani linaweza kuathiri uendeshaji wa viwanda hivyo kwa kukosa fedha hata za kununulia malighafi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ililiagiza Shirika la Nyumba Zanzibar kuanzisha miradi ya ujenzi wa nyumba mpya badala ya kutumia fedha kurekebisha nyumba za zamani. Katika utekelezaji wa agizo hili, Shirika limebuni miradi mipya ya ujenzi Mombasa – Unguja na Mabatini na Kilimatende kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa miradi hiyo bado haijaanza, Kamati inasisitiza Shirika kuanza utekelezaji wake katika mwaka huu wa fedha 2022/2023 kama Shirika lilivyoahidi mbele ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Uchapishaji unaotekelezwa na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Kamati iliagiza kuharakishwa kwa taratibu za manunuzi ya mitambo ya uchapaji. Katika utekelezaji wa agizo hilo, Kamati imearifiwa kwamba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilifunga mkataba na Kampuni ya Spicer mnamo tarehe 24 Februari, 2022 pamoja na kuwasilisha barua ya maombi ya fedha kwa Afisi ya Rais - Fedha na Mipango tokea tarehe 7 Machi, 2022. Hata hivyo, hadi sasa fedha hizo hazijapatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuwa makini na taratibu za manunuzi pamoja na kuhakikisha inasimamia vyema mikataba iliyoingia na wazabuni. Kutokutekeleza matakwa ya mikataba, kunaweza kupelekea kuitia hasara Serikali iwapo itapelekwa katika vyombo vya sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, Kamati inaitaka Serikali licha ya kutoa majibu na ufafanuzi mzuri unaohusiana na utekelezaji wa maagizo ya Kamati lakini kwa yale masuala ambayo bado utekelezaji wake haujakamilika ihakikishe inazisimamia taasisi zake ili ziweze kukamilisha utekelezaji wa maagizo hayo kwa wakati na kwa ufanisi.


## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa Serikali kuwasilisha majibu ya maagizo ya Kamati mbele ya Baraza ni matakwa ya Kanuni ya 109 (17) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020). Jambo hili ni zuri sana kwani chombo hichi kinapata mrejesho wa maagizo yaliyotolewa na Kamati kupitia Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti inapenda kuzipongeza kwa dhati Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri za kuisimamia Serikali katika kuhakikisha ufanisi wa majukumu ya chombo hichi unapatikana. Aidha, Kamati inaisisitiza tena Serikali kupitia taasisi mbali mbali kutekeleza sehemu ya maagizo na ushauri wa Kamati ambayo bado hayajatekelezwa ili lengo la kufanya kazi kwa pamoja la kuwatumikia wananchi liweze kufikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante



…………………….

Miraji Khamis Mussa,

Kny: Mwenyekiti,

Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**